# Utafiti wa binadamu na mazingira mikoa ya kati Tanzania

Namba 12

## MADAH
## UJENZI WA JAMII MPYA

Wilhelm Östberg

SUA LIBRARY
SPECIAL COLLECTION

Imetolewa na EDSU na IRA

STOCKHOLM UNIVERSITY 1994 UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM

Mpango wa utafiti wa Binadamu na Mazingira Mikoa ya Kati Tanzania unaendeshwa kwa ushirikiano kati ya Institute of Resource Assessment (IRA), Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, nchini Tanzania, na Environment and Development Studies Unit (EDSU), School of Geography, Stockholm University, Sweden.

Watafiti wapatao kumi na tano kutoka nyanja mbalimbali wanahusika na utafiti huu. Vyuo hivyo viwili vinashirikiana katika mipango mbalimbali ya kuandaa na kutekeleza shughuli za utafiti. Mpango huu unaratibiwa na Mkurugenzi wa IRA, Profesa Idris Kikula na Mkuu wa kitengo cha EDSU, Profesa Carl Christiansson. Fedha kwa ajili ya mpango huu zimetolewa na the Swedish Agency for Research Cooperation with the Developing Countries, SAREC.

Matokeo ya utafiti huu yanatarajiwa kutumika na idara mbalimbali za serikali na mashirika ya umma,miradi ya Hifadhi Ardhi na Mazingira na mashirika mbalimbali ya kimataifa yaliyo katika mikoa hiyo. Wakati huo huo matokeo ya utafiti huo yatasaidia katika kuelewa hali halisi ya mazingira na matumizi ya ardhi katika mikoa inayohusika.

Makala haya yana taarifa ya utafiti uliofanyika katika kuchangia mpango huo. Orodha ya makala mengine yanayohusiana na mpango huo wa utafiti yanapatikana kutoka Institute of Resource Assessment, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, S.L.P.35097, Dar-es-salaam au kutoka the Environment and Development Studies, School of Geography, Stockholm University, S-106 91 Stockholm, Sweden.

Tafsiri: Maandishi haya yametafsiriwa katika Kiswahili na Mary Mung' ong'o.

ISSN 1104-5299

2015 July

# MADAH
## Ujenzi wa Jamii Mpya

Makala ya Wilhelm Östberg

Madah ni jumuia inayopanuka kwa kasi sana. Hapo awali jumuia hii ilikuwa ni kitongoji cha kijiji cha Songolo, wilayani Kondoa. Sasa hivi jumuia hiyo inainukia kwa haraka kuwa jumuia yenye umaarufu wa pekee. Kamati iliyochaguliwa na wakazi wa hapo Madah sasa ndiyo inapanga na kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kijitabu hiki kinaelezea historia ya Madah na kinajaribu kutoa picha ya hali ya mambo kama yalivyokuwa mwaka 1993.

### Wakazi wa Asili

Madah iko katika eneo la Burunge. Kwa muda mrefu eneo hili lilikaliwa na familia chache za Kiburunge. Wamasai walileta mifugo yao kwa musimu lakini watu waliojenga makazi ya kudumu hapo Madah ni Waburunge. Mzee Medha ambaye sasa hivi ana umri wa miaka kama sabini hivi, alizaliwa Madah katika sehemu iliyo chini ya mlima. Mzee Medha alipokuwa mdogo wazazi wake walihamahama katika sehemu mbalimbali za Madah kwa sababu Waburunge wana kawaida ya kufuata mahali palipo na pori ili waweze kufyeka na kufanya makazi.

Mwaka 1974 wakazi wote wa Madah walihamishwa kufuatia mwito wa Oparesheni Vijiji, lakini baadhi ya watu waliohama waliendelea kulima katika eneo la Madah ingawa walikuwa wanaishi katika vijiji vya Chandama au Songolo. Baada ya muda mfupi msitu na wanyama pori vikatawala sehemu kubwa ya Madah. Leo Mzee Medha ni kati ya wazee wachache walioshuhudia mabadiliko ya muda mrefu ya Madah. Wakazi wengi wanaoishi Madah sasa hivi ni watu ambao wamehamia hapo katika kipindi cha miaka kumi tu iliyopita.

### Uhamiaji Madah


Watu wa kijiji cha Songolo walilifahamu vizuri eneo la Madah kwa sababu walikuwa wanachunga mifugo yao huko na kuinywesha kwenye bwawa la Madah. Kadiri miaka ya 1970 ilivyosonga mbele na uongozi kulegeza sheria za kuwabana watu wabaki katika vijiji vipya, baadhi ya watu walianza kuwaza juu ya kuhamia Madah. Mwaka 1981 watu sita kutoka kijiji cha Songolo walianza kufyeka msitu wa Madah kwa madhumuni ya kuhamia. Baada ya muda, watu wanne kati yao walighairi baada ya kushindwa kuondoa miti mikubwa kutoka kwenye maeneo waliyofyeka. Mwaka 1982 familia mbili zilihamia Madah. Katika mwaka

SOKOINE UNIVERSITY OF AGR. LIBRARY

huo huo na mwaka uliofuata watu wengine pia walianza kufyeka msitu wa Madah. Waanzilishi wa eneo hilo la Madah bado wanakumbuka jinsi walivyokuwa wakifyeka mpaka majira ya saa kumi na moja adhuhuri ndipo waanze kutimua mbio za kurudi kijijini Songolo kabla wanyama pori hawajaanza kuzungukazunguka kadiri jioni ilivyokaribia. Wenyewe wanasema, "Tulikuwa kama mifugo inayokimbia ikifuatwa na wanyama wakali".

Hatua kwa hatua idadi hiyo ndogo ya wahamiaji iliendelea kujijenga. Mwaka 1986 kituo kilijitokeza karibu na miamba katika eneo la Madah. Mahali hapo ndipo palipoonekana kuwa panafaa kwa ujenzi wa makazi. Nyumba zilizojengwa zilikuwa kama mpaka kati ya wanyama pori walio msituni na eneo la mashamba. Hali ya hewa ya eneo hili ni nzuri kwa sababu eneo liko katika sehemu iliyoinuka yenye vivuli vya miti na mlima. Eneo hilo halina hatari yoyote ya kukumbwa na mafuriko ikilinganishwa na maeneo la bondeni.

Mwaka 1989 Madah ilifanywa kitongoji cha kijiji cha Songolo. Wakazi walianza kufikiria juu ya kujenga shule na pia kuanzisha tawi lao la



Mzee Medha, mmoja wa Waburunge maarufu katika kijiji cha Madah. Yeye ni kati ya wazee wachache sana waliozaliwa hapo Madah.



chama. Majadiliano yalianza kati ya viongozi wa kijiji cha Songolo na viongozi wa wilaya ya Kondoa. Eneo la Madah lilikuwa mbioni kuelekea kwenye jumuia yenye matumaini ya mafanikio makubwa.

## Wahamiaji

Warangi waliopo wamekuwa wakiishi katika sehemu mbalimbali kabla ya kufika hapo Madah. Wamekuwa wakihamahama kutoka Milima ya Kondoa Irangi kuelekea kwenye vijiji vilivyo katika mbuga mashariki mwa vilima vya Mrijo, Itolwa au Kinyasi; kaskazini na mashariki mwa vilima vya Uburunge. Ingawa kwa sasa hivi wameamua kutulia na kujijenga hapo Madah, bado wanamiliki mashamba katika vijiji hivyo vingine. Ingawa asili yao ni katika bonde la Haubi, eneo hilo halina kivutio zaidi kwa hivi sasa na Milima ya Kondoa Irangi ni mahali ambako wanatembelea kwa nadra tu kuona ndugu ama kutambika.

Watu wengi waliohamia Madah wana matumaini makubwa sana ya maendeleo. Walipofika hapo kijijini kwa mara ya kwanza walikuwa na kawaida ya kuazima mashamba kutoka kwa wakazi waliotangulia kuhamia hapo. Wakati huo huo walianza pia kufyeka mashamba yao mapya. Wengi wa wahamiaji hao ni watu ambao wameikimbia ardhi iliyoharibika kupita kiasi. Vile vile wametoka katika maeneo yenye uhaba mkubwa wa mavuno na ufinyu wa ardhi ya kulima. Kwa kadiri familia zao zinavyozidi kupanuka wanalazimika kuhama na kutafuta sehemu yenye nafasi ya ardhi. Hivyo ndivyo wengi walivyofika Madah.

Eneo la Madah liko tofauti kabisa na maeneo mengine kwa sababu hata kama mwaka ni mbaya kwa mavuno lakini bado watu watakuwa na chakula cha kutosha, tofauti na hali ilivyo katika kijiji cha Kinyasi. Ali Iddy Suleiman alifika kwa mara ya kwanza hapo Madah kama utingo wa lori lililokuja kununua mazao hapo kijijini. Hali nzuri ya mavuno aliyoiona hapo kijijini ilikuwa kishawishi kikubwa kilichomfanya aache kazi ya utingo na kuhamia Madah. Alifika hapo kijijini kwa madhumuni ya kuhamia mwezi Januari mwaka 1991. Alipewa banda la kuishi pamoja na shamba lenye ukubwa wa ekari tano ambalo angelima kwa muda wa miaka mitatu. Kwa haraka sana alifyeka ekari nyingine tatu, hivyo akawa na jumla ya ekari nane. Mke wake na watoto sita nao wamehama kutoka kijiji cha Kinyasi na kuungana naye hapo Madah ambako wanayafurahia sana maisha yao mapya. Wamekaribishwa vizuri na majirani na wana uhakika kabisa kuwa maisha yao hapa yatakuwa bora zaidi kuliko kama wangeendelea kuishi huko Kinyasi. Kwa furaha waliyo nayo wanaona hakuna mahali panapofaa kuishi zaidi ya Madah.

Baadhi ya familia zilizotoka Milima ya Kondoa Irangi zina mpango wa kuishi hapo Madah kwa muda ili waone kama hali ya maisha itabadilika. Wao wanadai kuwa ingawa hali ya mavuno ni nzuri lakini ni porini mno.

Warangi hao wanayakumbuka sana maisha ya kwao yenye starehe za kila namna. Wanayakumbuka magulio ya kila Jumapili huko Haubi, vile vile wanayakumbuka mashamba yao yaliyoshehena kila aina ya matunda, bila kuzisahau bustani zao zilizojaa kila aina ya mboga za majani. Kijana mmoja mwenye umri wa kama miaka ishirini ambaye amehamia hivi karibuni hapo kijijini, anaamini kuwa baada ya kuishi hapo kwa miaka mitatu atakuwa mtu maarufu, na kwamba atakuwa amekwisha kuwa na uwezo wa kuanzisha biashara.

Kundi jingine la wahamiaji wa Madah ni Wabarabaig. Wao wanajitahidi kudumisha uhusiano wao na wilaya ya Hanang na pia wanahusiana na makundi mengine ya Wabarabaig yaliyosambaa katika sehemu mbalimbali za wilaya ya Kondoa na Babati. Sheria za makazi zilipoanza kulegalega wakati wa Oparesheni Vijiji mwishoni mwa miaka ya 1970, baadhi ya Wabarabaig walihamia hapo Madah. Baadaye Wabarabaig wengine walihamia hapo kutoka Bubu, Busi, Masange na sehemu nyingine katika jitihada za kutafuta mashamba na malisho ya mifugo yao.



Katika eneo la Madah wakazi wamejenga nyumba zao karibu na miamba ya mawe na kutumia maeneo ya mabondeni kwa shughuli za kilimo. Nyumba hizo zinatengeneza mpaka kati ya wanyama pori wanaoishi msituni na mashamba.



## Ongezeko la Idadi ya Watu

Mwaka 1989 Madah ilikuwa na kaya 111. Idadi hiyo iliendelea kuongezeka na hadi kufikia mwezi Mei, 1992 kulikuwa na kaya 142. Kufikia mwishoni mwa mwaka tayari kulikuwa na kaya zipatazo 169. Katika idadi hiyo kaya 105 zilikuwa ni za Warangi, kaya 40 za Waburunge, kaya 20 za Wabarabaig, na kaya 3 za Wagogo. Kadhalika kulikuwa na kaya 1 ya Wairaqw. Kutokana na takwimu hizo ni dhahiri kuwa kulikuwa na ongezeko kubwa sana la watu.

Takwimu zilizoonyeshwa hapo juu ni za wakazi walioandikishwa tu. Wahamiaji wapya hufahamika baada ya kitambo cha muda kupita na vile vile kuna hali ya watu wengi kuingia na kutoka hapo kijijini, hivyo si rahisi kujua kwa haraka tofauti kati ya mkazi na mpita-njia. Mfano hai ni wa Wabarabaig ambao wanaweza kujenga boma la mapumziko ya miezi michache kabla ya kuendelea na safari zao.

## Upatikanaji wa Mashamba


Uongozi wa Madah uko mbioni kuzuia ufyekaji holela wa msitu. Uongozi huo umeamua kuwa mashamba mapya yatakuwa na ukubwa wa ekari tatu hadi ekari tano. Uongozi huo unahofia kwamba wasipofanya hivyo wageni watamiliki sehemu kubwa ya mashamba mapya na kwamba wanaweza kuanzisha miradi kama vile kuuza mashamba hayo ambayo wao waliyapata bure. Iwapo mgeni atakuwa nao watoto wawili au zaidi basi atapewa ekari sita. Baadaye wageni hao wanaweza kuongezewa maeneo kufuatana na mahitaji. Mlinzi wa msitu wa hapo Madah ana jukumu kubwa la kutoa ushauri kwa wahamiaji juu ya miti ambayo hawaruhusiwi kuikata na kwamba ufyekaji wa mashamba hayo hautaathiri hali ya mazingira kwa njia yoyote.

Ye yote anayehamia Madah analazimika kuomba msaada wa shamba na makazi ya muda kutoka kwa ndugu au jamaa ambao wamekwisha kujijenga hapo kijijini. Baada ya muda mgeni huyo hutambulishwa kwa kamati ya uongozi ya hapo Madah ili aweze kugawiwa eneo la kufyeka. Hata hivyo kuna baadhi ya wageni ambao wanakuja hapo kijijini na vibali vya kufyeka msitu vinavyotolewa na serikali ya kijiji cha Songolo.

Hapo awali madaraka ya kugawa ardhi yalikuwa mikononi mwa serikali ya kijiji cha Songolo, sasa madaraka hayo yameachwa mikononi mwa kamati ya uongozi inayowawakilisha wakazi wengi wa Madah. Madah ambayo hapo mwanzo ilikuwa ni sehemu ndogo tu ya msitu uliofyekwa sasa hivi inainukia kuwa jumuia kamili yenye sheria na taratibu zake.

**Shule**
Wakazi wa Madah waliona kuwa kuna umuhimu wa kuwa na shule yao wenyewe. Mwaka 1990 Madah ilikuwa na watoto 260 waliokuwa na umri chini ya miaka 12. Wengi wa watoto hao walibaki tu nyumbani wakati baadhi yao walitembea mwendo mrefu kwenda na kurudi ili waweze kuhudhuria shule iliyo katika kijiji cha Songolo. Wazazi walijenga jengo hafifu la asili likiwa na chumba kimoja cha darasa na mabenchi kadhaa ya kukalia. Waliomba shule yao isajiliwe ili iweze kupangiwa mwalimu kutoka wilayani. Uongozi ulikataa maombi ya kuisajili shule hiyo mara mbili. Muda huo wote walimu wa kujitolea walianza kufundisha. Walimu wa mwanzo kabisa walitokana na kamati ya uongozi ambao walikuwa ni Katibu wa kamati hiyo, Bwana Juma Nkuri, na Bwana Karimu Ramadhani.

Mwezi August mwaka 1991 wazazi walianza kufyatua matofali kwa ajili ya ujenzi wa darasa jipya. Hatimaye Afisaelimu wa wilaya alitambua juhudi za wazazi za kuanzisha shule kamili hapo Madah na Bwana Halfani Chimbalambala kutoka Goima, mwalimu aliyekuwa na uzoefu wa miaka



Shule ya Madah ilivyokuwa mwezi Mei, 1992. Aliyesimama upande wa kulia ni Mwalimu Mkuu wa shule hiyo Bwana Halfan Chimbalambala.



kumi na moja ya kufundisha, alichaguliwa kuwa mwalimu mkuu wa shule mpya ya Madah.

Mwaka 1993 wanafunzi 51 waliandikishwa darasa la kwanza. Kati ya hao 23 walikuwa wasichana na 28 walikuwa wavulana. Darasa la pili lilikuwa na wanafunzi 41 ambao 23 kati yao walikuwa wavulana na 18 wasichana. Wanafunzi wachache wa madarasa ya juu wa hapo Madah waliendelea kuhudhuria masomo yao huko Songolo.

Mafunzo ya madras pia yanatolewa hapo Madah katika msikiti mdogo uliojengwa mwaka 1988. Walimu wawili wa kujitolea wanaendesha shughuli hiyo.

**Serikali ya Madah**
Serikali ya kwanza ya kijiji hapo Madah iliundwa mwaka 1989 na kisha kamati ikachaguliwa ili kusimamia ukarabati wa barabara ya kwenda



Hii ni Kamati ya mwanzo kabisa iliyoandaa na kusimamia shughuli mbalimbali za maendeleo hapo kijijini Madah. Aliyekaa upande wa kushoto ni Katibu wa kamati hiyo, Bwana Juma Nkuri, na pembeni kwake, aliyeshika kalamu ni Mwenyekiti wa kamati hiyo, Bwana Hatibu Hamisi Nyodi.

Songolo. Kutokana na hali nzuri ya mavuno wakazi wengi waliona umuhimu wa kuwa na barabara nzuri ili waweze kusafirisha mazao yao. Kamati hiyo ndiyo iliyosimamia ujenzi na uanzishaji wa shule ya hapo Madah. Ni kamati hiyo pia iliyochangia kwa kiasi kikubwa katika kuhamasisha wakazi wengine na kuwezesha usajili wa tawi lao la CCM. Kamati hiyo ina wajumbe kumi ambao walichaguliwa katika mkutano wa wakazi wote ambapo kila mwanachama wa CCM aliruhusiwa kupiga kura moja tu. Wajumbe watano kati ya hao kumi, ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti, Bwana Rashid Sauri Busi, na Katibu, Bwana Juma Nkuri wanafanya kamati ya siasa. Kamati nzima inashirikiana bega kwa bega na balozi ili kufanikisha shughuli mbalimbali za hapo Madah. Wajumbe wote wa kamati ya siasa ni Warangi.

**Matumizi ya Ardhi**
Warangi wanaishi katika eneo la katikati ya Madah. Waburunge wengi wanaishi sehemu za miinuko zilizoko upande wa Kusini. Baadhi ya Wabarabaig wanaishi pembezoni mwa Madah wakati ambapo wengine wanaishi Chambogo katika eneo la kaskazini. Denesa ambalo ni eneo lililo upande wa Magharibi hutumiwa zaidi kwa kuchungia mifugo. Eneo linalokaliwa na Waburunge lina msongamano wa watu wakati ambapo bado kuna nafasi kwa ajili ya wahamiaji wapya katika sehemu nyingine za Madah.

Baadhi ya wakazi wa Kirangi wanalima mashamba yenye ukubwa wa ekari 40 mpaka 60 kwa kutumia jembe la ng'ombe au trekta. Lakini kaya nyingi za Kirangi zina mashamba yenye ukubwa wa kawaida, kati ya ekari 10 na ekari 30. Mara nyingi hao wenye mashamba madogo ni wageni ambao wamehamia hapo kijijini hivi karibuni. Mtindo unaotumika wakati wa kuandaa mashamba hayo ni ule wa kulima na kupanda kwa wakati mmoja. Kutokana na uzito wa shughuli ya kulima na kupanda watu wengi hulima kwa kushirikiana.

Kwa sababu karibu Warangi wote hulima kwa jembe la ng'ombe au trekta mashamba yao huwa ni makubwa sana yakilinganishwa na mashamba ya Waburunge ambao hawatumii jembe la ng'ombe wala trekta. Wabarabaig wote wanaoishi Madah wanalima na wengi wao hutumia jembe la ng'ombe.

**Mazao**
Mazao makuu yanayolimwa Madah ni mahindi, mtama mwekundu, ulezi na uwele. Sehemu kubwa ya mazao hayo yanasafirishwa. Wafanya biashara wanaotoka Arushi, Moshi na Kondoa wananunua zaidi ulezi wakati ambapo mahindi na mtama mwekundu hununuliwa zaidi na wafanya biashara kutoka Dodoma. Mazao mengine yanayolimwa ni maharage na karanga. Zao la muhogo nalo limeanza kuwa maarafu. Kunde na mbaazi ni mazao yanayolimwa kwa ajili ya matumizi ya



nyumbani, ikiwa ni pamoja na vitunguu, nyanya na aina mbalimbali za mboga za majani. Katika sehemu hiyo hakuna miti yoyote ya matunda isipokuwa mizambarau michache tu.

**Biashara ya Ulezi**
Moja ya vivutio vya Madah ni uwezekano wa kilimo cha zao la ulezi. Katika eneo hili udongo una rutuba na mvua ni za uhakika zaidi kuliko hali ilivyo huko mbugani.

Bei ya zao la ulezi ni mara mbili ya bei ya nafaka nyingine. Faida nyingine ya kilimo cha zao la ulezi ni kwamba halihitaji gharama yoyote



Akina mama wanatwanga uwele.

Songolo. Kutokana na hali nzuri ya mavuno wakazi wengi waliona umuhimu wa kuwa na barabara nzuri ili waweze kusafirisha mazao yao. Kamati hiyo ndiyo iliyosimamia ujenzi na uanzishaji wa shule ya hapo Madah. Ni kamati hiyo pia iliyochangia kwa kiasi kikubwa katika kuhamasisha wakazi wengine na kuwezesha usajili wa tawi lao la CCM. Kamati hiyo ina wajumbe kumi ambao walichaguliwa katika mkutano wa wakazi wote ambapo kila mwanachama wa CCM aliruhusiwa kupiga kura moja tu. Wajumbe watano kati ya hao kumi, ikiwa ni pamoja na Mwenyekiti, Bwana Rashid Sauri Busi, na Katibu, Bwana Juma Nkuri wanafanya kamati ya siasa. Kamati nzima inashirikiana bega kwa bega na balozi ili kufanikisha shughuli mbalimbali za hapo Madah. Wajumbe wote wa kamati ya siasa ni Warangi.

**Matumizi ya Ardhi**
Warangi wanaishi katika eneo la katikati ya Madah. Waburunge wengi wanaishi sehemu za miinuko zilizoko upande wa Kusini. Baadhi ya Wabarabaig wanaishi pembezoni mwa Madah wakati ambapo wengine wanaishi Chambogo katika eneo la kaskazini. Denesa ambalo ni eneo lililo upande wa Magharibi hutumiwa zaidi kwa kuchungia mifugo. Eneo linalokaliwa na Waburunge lina msongamano wa watu wakati ambapo bado kuna nafasi kwa ajili ya wahamiaji wapya katika sehemu nyingine za Madah.

Baadhi ya wakazi wa Kirangi wanalima mashamba yenye ukubwa wa ekari 40 mpaka 60 kwa kutumia jembe la ng'ombe au trekta. Lakini kaya nyingi za Kirangi zina mashamba yenye ukubwa wa kawaida, kati ya ekari 10 na ekari 30. Mara nyingi hao wenye mashamba madogo ni wageni ambao wamehamia hapo kijijini hivi karibuni. Mtindo unaotumika wakati wa kuandaa mashamba hayo ni ule wa kulima na kupanda kwa wakati mmoja. Kutokana na uzito wa shughuli ya kulima na kupanda watu wengi hulima kwa kushirikiana.

Kwa sababu karibu Warangi wote hulima kwa jembe la ng'ombe au trekta mashamba yao huwa ni makubwa sana yakilinganishwa na mashamba ya Waburunge ambao hawatumii jembe la ng'ombe wala trekta. Wabarabaig wote wanaoishi Madah wanalima na wengi wao hutumia jembe la ng'ombe.

**Mazao**
Mazao makuu yanayolimwa Madah ni mahindi, mtama mwekundu, ulezi na uwele. Sehemu kubwa ya mazao hayo yanasafirishwa. Wafanya biashara wanaotoka Arushi, Moshi na Kondoa wananunua zaidi ulezi wakati ambapo mahindi na mtama mwekundu hununuliwa zaidi na wafanya biashara kutoka Dodoma. Mazao mengine yanayolimwa ni maharage na karanga. Zao la muhogo nalo limeanza kuwa maarafu. Kunde na mbaazi ni mazao yanayolimwa kwa ajili ya matumizi ya



nyumbani, ikiwa ni pamoja na vitunguu, nyanya na aina mbalimbali za mboga za majani. Katika sehemu hiyo hakuna miti yoyote ya matunda isipokuwa mizambarau michache tu.

**Biashara ya Ulezi**
Moja ya vivutio vya Madah ni uwezekano wa kilimo cha zao la ulezi. Katika eneo hili udongo una rutuba na mvua ni za uhakika zaidi kuliko hali ilivyo huko mbugani.

Bei ya zao la ulezi ni mara mbili ya bei ya nafaka nyingine. Faida nyingine ya kilimo cha zao la ulezi ni kwamba halihitaji gharama yoyote



Akina mama wanatwanga uwele.

kuliuza. Wafanya biashara kutoka Haubi, Kondoa, Arusha na Moshi wanalifuata zao hilo hadi huko mashambani. Mahitaji makubwa ya zao la ulezi yanamfanya mkulima awe na kauli ya kupanga bei anayotaka. Zao la ulezi ni zao ambalo ni rahisi kulihifadhi ghalani endapo njaa itatokea. Hivyo ni zao lisilohitaji haraka ya kuliuza. Tatizo kubwa la kilimo cha zao la ulezi ni kwamba wakulima wanaogundua faida kubwa inayopatikana kutokana na zao hilo hawazingatii tena athari za uharibifu wa ardhi. Wao wanachojali ni kuvuna faida yote inayoweza kupatikana bila kujali mambo ya uharibifu wa udongo. Ardhi ya umma inageuzwa kuwa chombo cha kuwanufaisha watu wachache ambao hatimaye hupeleka faida hiyo mahali pengine.

**Mifugo**
Karibu nusu ya Warangi wanaoishi Madah wana mifugo kati ya ng'ombe watano hadi kufikia ng'ombe ishirini. Wakulima wasio na mifugo yao wenyewe hutumia mbinu ya kununua majembe ya ng'ombe na kuazimisha ili nao waweze kulimiwa mashamba yao. Vile vile wanaweza kulimiwa mashamba yao kwa jembe la ng'ombe kwa gharama ya shilingi 2,000/= kwa kila ekari au kukodi trekta kwa gharama ya shilingi 3,500/= kila ekari.

Wabarabaig pia wana mifugo. Mifugo hiyo imetawanywa katika sehemu mbalimbali hasa wakati wa msimu wa kilimo. Wabarabaig wanaoishi Madah wanajieleza kuwa wana idadi ndogo ya mifugo hapo kijijini ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya mboga tu. Wabarabaig hao hutumia fedha zao zote zinazopatikana kutokana na kilimo kununua mifugo.

Waburunge wana mifugo michache sana. Wao wanapata fedha kwa kurina na kuuza asali.

**Zao la asali**
Wakazi wa Madah wana uwezo wa kuinua hali zao za maisha kwa kuchonga mizinga na kufuga nyuki. Ni jambo la kawaida kabisa kwa wakazi wa Madah kuwa na mizinga kadhaa, na asali ni zao mojawapo linaliwapatia fedha za kutosha kabisa. Utengenezaji wa pombe ya asali ni moja ya mambo yanayowajumuisha wakazi na vile vile pombe ya asali ni moja ya mahitaji muhimu katika shughuli za matambiko na burudani ya kawaida, hasa kwa Wabarabaig.

**Hali ya Mazingira**
Watu waliohamia Madah mwanzoni mwa miaka ya 1980 walijiamulia wenyewe mahali wanapotaka kufyeka mashamba yao. Kwa kawaida Waburunge wana mtindo wa kuhifadhi miti mikubwa, lakini kwa sababu miti hiyo ilikuwa imeota kiholela humo msituni wahamiaji waliikata bila kujali utaratibu huo wa kuihifadhi, isipokuwa kwa miti iliyokuwa na mizinga. Jinsi idadi ya wahamiaji ilivyozidi kuongezeka Waburunge wa



Madah walilazimika kuirudia kawaida yao ya mwanzo ya kuwaelekeza wageni maeneo ambayo yanatakiwa kuhifadhiwa, kama vile maeneo ya makaburi, na kwamba aina fulani fulani za miti haziruhusiwi kukatwa. Mfano hai wa miti inayohifadhiwa ni miti aina ya megea iliyo kando kando mwa kijito kinachopita katikati ya kijiji cha Madah ambayo sasa inatumika kama alama ya mahali.

Korongo kubwa linapita katikati ya Madah pembezoni mwa miti hiyo ya megea. Barabara inapita katikati ya korongo hilo ambalo lilitokea baada ya watu kuanza kulima katika mteremko kuelekea mlimani. Kingamaji kubwa lilikuwa limetengenezwa ili kuzuia maji yanayotoka kwenye maeneo yaliyofyekwa sehemu za mwinuko yasitiririke kwa kasi kubwa na kuzoa kila kitu kutoka kwenye mashamba yaliyo bondeni. Kingamaji hilo lilipobomoka udongo wote ulizolewa, kukabaki korongo hilo kubwa.

Hapo Madah kuna maeneo makubwa sana yaliyofyekwa. Katika sehemu ya katikati ya Madah kuna uoto kidogo sana. Kwa sababu wakulima wengi wanalima kwa jembe la ng'ombe ni miti michache sana inaachwa mashambani. Kamati ya siasa imetunga baadhi ya sheria ndogo ndogo zinazosaidia kuhifadhi mazingira. Vile vile sheria hizo zinazuia kuchunga mifugo katika eneo la shule. Pia mifugo hairuhusiwi kunyweshwa kwenye visima viwili ambavyo maji yake ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Mlinzi wa msitu anajitahidi sana kuonyesha aina ya miti inayotakiwa kuhifadhiwa wakati wa ufyekaji wa mashamba, kama vile miti aina ya mpingo na mingine mingine ambayo inaweza kuuzwa kwa bei kubwa.

Afisa ardhi wa tarafa ya Goima amelikagua eneo la Madah na kuelekeza sehemu ambazo haziruhusiwi kuendelea kuchungia mifugo kutokana na hatari ya maeneo hayo kuharibika. Alimshauri mlinzi wa msitu kuwa jumla ya miti ipatayo 5,000 inatakiwa ipandwe katika miteremko ya vilima ili kuzuia mmomonyoko wa udongo katika miteremko hiyo. Afisa misitu wa wilaya alitembelea Madah mwaka 1993 ili kujadili suala la upandaji miti na kuangalia uwezekano wa kuanzisha kitalu cha miche ya miti katika eneo hilo.

**Maji kwa Matumizi ya Binadamu na Wanyama**
Visima vya maji vya Madah vinatoa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kipindi kikubwa cha mwaka. Lakini katika miaka yenye uhaba wa mvua visima hivyo hukauka baada ya ukame wa muda mrefu. Katika kipindi kama hicho mifugo hunyweshwa kwenye visima vilivyoko Chioli katikati ya vilima vya Uburunge au kwenye visima vilivyoko huko Soya.

Miaka ya 1960 Madah ilikuwa na bwawa. Tangu bwawa hilo lilipobomoka wakazi wa Madah wamekuwa wakilazimika kwenda huko

Chandama (mwendo wa saa tatu) kufuata maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kwa kipindi cha mwaka visima vinapokauka. Kwa wale walio na punda suala la uhaba wa maji huwa ni tatizo linaliweza kutatuliwa kwa urahisi, lakini kwa wale wasio na punda suala hilo huwa na uzito wa aina ya pekee.

Mifugo inanyweshwa huko Chioli, Soya au katika mbuga za Denesa. Wakati wa kiangazi kila kisima kinakuwa na foleni ndefu sana za mifugo iliyoletwa kunyweshwa. Makundi makubwa ya mifugo ya watu matajiri kutoka wilayani Hanang huchanganyika na makundi ya Wamasai na Wabarabaig pamoja na mifugo ya wafugaji wa Madah na vijiji vya jirani.

**Umaarufu wa Madah**

Watu wengi wazima wanaoishi Madah wameishi pia sehemu nyingine kabla ya kuhamia hapo. Kwa hiyo ni rahisi kwao kulinganisha hali ya maisha ya hapo Madah na ya hizo sehemu nyingine. Kwa sababu wengi wa wahamiaji wa Madah wanatoka katika sehemu zilizokumbwa na uharibifu mkubwa wa ardhi sio ajabu kusikia watu hao wanaisifia sana Madah.



Ufyatuaji wa matofali kijijini Madah.



Madah imeshehena uoto na kivuli cha msitu, ina udongo wenye rutuba na hali ya hewa ya kupendeza kuliko vijiji vya jirani. Miaka 1990 hadi 1993 ilikuwa ni miaka ya ukame; bado wakazi wa Madah waliweza kupata mavuno mazuri. Mjumbe mmoja wa kamati ya CCM anaisifu Madah kwa kusema, "Hatuna miaka ya umaskini hapa, hata kukiwa na uhaba wa mvua lakini bado Madah tunakuwa na mavuno ya kutosha. Mwaka 1989 ulikuwa ni mwaka mzuri sana kwa hali ya mazao. Tulipata mavuno mengi kiasi kwamba watu walikuwa wanalala juu ya magunia ya ulezi. Hatukuwa na maghala ya kutosha mavuno yote.Hata mwaka wa nyuma yake baadhi ya watu walipata zaidi ya magunia mia moja ya ulezi na magunia mara mbili ya hayo ya zao la mahindi".

**Tumaini la Maendeleo**

Baada ya tawi lao la CCM kusajiliwa, Katibu wa CCM wa tawi hilo kwa majivuno alisema, "Madah imejulikana sasa. Wafanya biashara wamegundua kuwa chakula kinapatikana kwa wingi hapa. Tutakapotengeneza barabara yetu mpya ya kwenda Soya itakuwa rahisi sana kufika Madah, kwa hiyo biashara itaongezeka. Labda hata basi la kutoka Mwailanje litaitumia barabara yetu mpya kama njia ya mkato ya kufika Goima na Kondoa". Wakazi wa Madah wameanza kujenga kutuo cha afya hapo kijijini.

Katika matukio mawili tofauti, kwenye mkusanyiko wa watu usio rasmi, tulijaribu kuwaambia wakazi hao waorodheshe matatizo makubwa yanayowakabili kijijini hapo. Tatizo la kwanza lililotolewa na wakazi wengi ni suala la matibabu. Ni kweli kwamba tatizo hilo ni kubwa kwa sababu zahanati zilizo jirani ziko Chandama na Hamai. Hata hivyo, mara nyingi zahanati hizo huishiwa madawa. Watu hulazimika kusafiri mpaka Goima au Mirambu ambako kuna zahanati zinazomilikiwa na mashirika ya dini au kwenda mpaka Kondoa mjini ili kuweza kupata matibabu.

Tatizo lao la pili ni ukosefu wa mashine ya kusaga nafaka. Tatizo la tatu ni suala la upatikanaji wa maji, wakati tatizo la nne ni suala la usafiri. Matatizo mengine yaliyoorodheshwa ni pamoja na upungufu wa majembe ya ng'ombe, ukosefu wa madawa ya mifugo, uhaba wa miti ya matunda na mengine mengi madogo madogo. Katika orodha hiyo walidokeza matatizo ambayo pia yanazikumba sehemu nyingine za wilaya ya Kondoa kama vile mmomonyoko wa udongo, ukosefu wa pembejeo na tatizo la upatikanaji wa masoko kwa ajili ya baadhi ya mazao.

Inafurahisha sana kusikia mafanikio yaliyofikiwa katika eneo la Madah na jinsi wakazi walivyopania kuitekeleza mipango yao mbalimbali ya maendeleo. Ni muhimu pia kujua kuwa kwenye miaka ya 1960 Madah ilikuwa na bwawa na pia kulikuwa na barabara iliyokwenda Kinando na Chambala ambayo inaunganisha na Chemba katika barabara kuu iendayo Dodoma na Arusha. Barabara inayopita katika vilima vya Uburunge

iliharibika na kubakia kama njia ya miguu kwa sababu ilikuwa haitumiki tena wakati wa Oparesheni Vijiji. Kwa maelezo mengine ni kwamba wakazi wa Madah wanafufua maendeleo ambayo yalikuwepo hapo kijijini tangu zamani.

**Maisha katika Jumuia.**

Baadhi ya wahamiaji wanakuwa na mashamba makubwa kwa madhumuni ya kuwarithisha watoto wao hapo baadaye, wakati ambapo wengine wameridhika na mashamba ya wastani tu. Hata hivyo, kuna wahamiaji wachache ambao wanalazimika kufanya vibarua vya muda ili kutosheleza mahitaji yao ya siku hata siku.

Wakulima wenye mafanikio mazuri wana ndugu au jamaa wengi wanaoishi nao hivyo ni rahisi kwao kumudu shughuli za kulima na kupanda. Wakati wa palizi na kuvuna mara nyingi wanatumia vibarua wa kutwa. Wakati mwingine shughuli zinakuwa nyingi kiasi ambacho inakuwa vigumu kupata vibarua wa kutosha kushughulikia mashamba ya ukubwa wa ekari arobaini mpaka ekari sitini. Lakini kwa bahati nzuri watu wanakuja wenyewe kutafuta kazi kutoka Goima na sehemu nyingine. Mara nyingi makubaliano na vibarua hao wanaotoka sehemu nyingine hufanyika kila Jumamosi kwenye gulio huko Songolo. Hali hiyo inawawezesha wakulima wa Madah kufanikisha shughuli zao za kulima na kuvuna bila migogoro ya kunyang'anyana vibarua. Kwa maana hiyo malipo ya vibarua hao yanabaki kuwa kidogo.

Madah ni jumuia inayobadilika haraka sana ambapo watu wanaweza kubadili hali zao za maisha na hata shughuli zao za maendeleo zinaonekana kuwa na mafanikio makubwa. Pamoja na maelezo hayo mazuri yaliyotolewa, Madah ni mahali ambapo tofauti kubwa miongoni mwa wakazi inaanza kujitokeza na vile vile kuna dalili za uharibifu wa ardhi zinazoanza kujitokeza.

**Je, Jumuia Inajitosheleza?**

Swali la kujiuliza ni je, Madah itaendelea kuwatosheleza wakazi wake kwa muda wote kama hali ilivyo hivi sasa? Kwa wastani mazingira ya Madah hayajafikia hali ya kutishiwa sana na mmomonyoko wa udongo, ingawa katika baadhi ya mashamba unaweza kuona mrundikano wa mchanga ulioachwa na maji yanayotiririka kupitia katika mashamba hayo. Baadhi ya mashamba yanayotunzwa vizuri yana kilimo cha matuta yanayokingama mteremko. Hata hivyo, mashamba mengi yanayolimwa kwa kutumia jembe la ng'ombe au kilimo cha sesa hali ya udongo na mbegu kuzolewa na maji ni jambo la kawaida. Katika maeneo kama hayo mimea inayobahatika kubakia hudumaa kwa kukosa udongo wenye rutuba. Katika sehemu zenye miteremko mikali zaidi matuta yanalimwa



kukingama mteremko ili kupunguza kasi ya maji na pia kuwezesha maji hayo kupita kwenye mifereji inayoachwa na matuta hayo.

Kwa maoni ya wakazi wa Madah, mmomonyoko wa udongo ni tatizo mojawapo linalowakabili. Wakati mwingine unaweza kuwasikia baadhi ya watu wakizungumzia juu ya hali inayoweza kutokea Madah hapo baadaye. Watu ambao wamekuwa wakiyaangalia mabadiliko ya Madah kwa muda mrefu kama Mzee Medha anajua kabisa ni nini kitatokea hapo baadaye. Wakati mwingine utamsikia akiuliza "Je, ni nani anayeweza kuamini kuwa kijiji cha Songolo zamani ulikuwa ni msitu tu? Hivi leo sehemu yote imebadilika na kuwa mbuga kubwa ya mashamba." Hali hiyo inaweza kutokea hata Madah.

Watu wanaendelea kumiminika Madah kutoka sehemu mbalimbali. Familia nyingi za Madah ni za vijana. Hali hii inaonyesha kuwa ongezeko la idadi ya watu litaendelea kuwa kubwa kadiri muda utakavyopita. Ongezeko la idadi ya watu na mifugo maana yake ni ongezeko la mahitaji mbalimbali yanayotokana na ardhi. Soko litaendelea kuhitaji mazao kutoka katika mashamba ya kijijini hapo. Ingawa zao la ulezi lina faida kubwa, hasara yake ni kwamba zao hilo linapoteza rutuba yote iliyo katika tabaka la juu la udongo. Hali hiyo inaashiria hatari ya upungufu wa mavuno hapo baadaye.
Familia chache za Madah hutumia muda wao mwingi kufanya vibarua katika mashamba ya wakulima wenye uwezo. Matokeo yake ni kwamba shughuli kidogo zinazofanyika katika mashamba yao zinafanywa kwa kuchelewa sana na kusababisha hali duni ya maisha ya watu hao kujirudia mwaka hata mwaka.

Baadhi ya wahamiaji ni wakazi wa muda tu wakiwa na lengo la kuchuma huku porini ili baadaye waweze kurudi mjini na hali ya utajiri. Watu kama hao hawana mpango wowote wa tahadhari ya uharibifu wa mazingira.

Wakulima wanaofanya biashara ya ulezi na miji ya Arusha na Moshi hawana muda wa kuhangaika na hifadhi ya ardhi. Nia yao ni kuvuna kwa haraka kila kinachowezekana kabla hali haijabadilika. Faida yote wanayoipata wanaitumia kuanzisha biashara katika sehemu nyingine.

Masuala hayo yote yaliyoelezwa hapo juu yanamfanya mtu awe na wasiwasi mkubwa juu ya hali ya baadaye ya kijiji cha Madah. Lakini kutokana na ukweli kwamba wakazi wa Madah wamegundua kuwepo kwa tatizo hilo la uharibifu wa ardhi bila shaka watajitahidi kwa juhudi zao zote kukabiliana nalo na kuchukua kila hatua za tahadhari ili kuzuia lisiendelee.

**Shukrani**

Nashukuru kwa kupokelewa vizuri hapo Madah na kupewa ushirikiano wa hali ya juu ulioturahisishia ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya kijitabu hiki. Tulipata kila msaada tuliouhitaji. Wazee walitueleza kinaganaga asili ya Madah, viongozi walitupa takwimu zote tulizozihitaji pamoja na kutueleza kwa kifupi mipango ya baadaye ya Madah. Wakulima walituelezea uzoefu wao wa shughuli za kilimo na maisha ya hapo kijijini kwa jumla, na vijana walijitolea kutuongoza katika ziara tulizozifanya kutembelea mashamba na hata ziara za msituni. Kutokana na hayo yote tuliyokirimiwa kutoka pande zote, si rahisi kumshukuru mtu mmoja mmoja kwa jina. Ni matumaini yangu kuwa kila mtu aliyechangia katika kufanikisha toleo hili atazipokea shukrani zangu za jumla na za dhati.

Utafiti huu ulifanywa kwa kushirikiana na Bwana Joseph Mduma, ambaye ni mtaalamu wa misitu anayeshughulika na mradi wa HADO. Natoa shukrani za dhati kwa ushirikiano nilioupata kutoka uongozi wa mradi, bila kumsahau Bwana Mduma binafsi kwa utaalamu wake na moyo wa kujituma uliochangia kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha shughuli hii. Kwa sababu zisizoweza kuzuilika imekuwa vigumu kushirikiana na Bwana Mduma katika uandaaji wa kijitabu hiki. Tumeshirikiana vizuri sana katika kufanya utafiti huu lakini makosa yoyote ambayo yanaweza kujitokeza katika toleo hili ni yangu mimi binafsi.



SOKOINE UNI OF AGR LIBRARY